# JOTOARDHI JARIDA



**KAMPUNI YA UENDELEZAJI JOTOARDHI TANZANIA**

# Utangulizi

Karibu kwenye Jotoardhi Jarida, chapisho rasmi linaloangazia maendeleo, fursa, na matukio yanayohusiana na sekta ya nishati hususan jotoardhi. Katika jarida hili, tunakuletea taarifa muhimu kuhusu miradi ya jotoardhi, sera za nishati, uvumbuzi wa kiteknolojia, na mchango wa sekta hii katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kupitia makala maalum, mahojiano na wataalamu, na uchambuzi wa kina, Jotoardhi Jarida linajenga uelewa wa kina kuhusu jinsi jotoardhi inavyoweza kuwa suluhisho endelevu kwa upatikanaji wa nishati safi na ya uhakika. Lengo letu ni kukuza uelewa, kushirikisha wadau, na kuhamasisha uwekezaji katika sekta hii yenye fursa tele.

Tunatumaini kuwa kila toleo la jarida hili litakuwa chachu ya majadiliano na hatua zinazolenga kuimarisha matumizi ya jotoardhi kwa maendeleo ya taifa letu. Karibu usome, ujifunze, na uhamasike.



## 01.

## Siku ya Wanawake wa TGDC: Furaha, Ushirikiano na Hamasa

Ilikuwa siku ya furaha na mshikamano kwa Malkia wa TGDC walipokutana katika ufukwe wa White Sands kusherehekea Siku ya Wanawake wa TGDC. Hafla hii iliwaleta pamoja kwa ajili ya kufurahia, kujifunza, na kuhamasishana katika safari yao ya maendeleo binafsi na ya kikazi.

Katika hotuba yake, Meneja Rasilimali Watu Mwandamizi, Bi. Judith Gowelle, aliwahimiza wanawake wa TGDC kujihusisha na shughuli mbalimbali za kimaendeleo ili kujiongezea kipato na kujenga maisha imara zaidi. Alisisitiza umuhimu wa kuwa na mipango endelevu itakayowawezesha wanawake kujitegemea na kuchangia maendeleo ya jamii.

Pamoja na hotuba hiyo yenye hamasa, siku ilijawa na mijadala yenye kuhamasisha, ushauri wa masuala mbalimbali ya maisha, na kubadilishana mawazo chanya. Pia, wanawake walipeana zawadi kama ishara








02.

## Siku ya Wanawake wa TGDC: Furaha, Ushirikiano na Hamasa

ya kuthamini juhudi na mchango wao katika kazi na jamii kwa ujumla.

Hakika, ilikuwa siku iliyofana sana, ikidhihirisha mshikamano na ari ya wanawake wa TGDC katika kufanikisha maendeleo. TGDC, Tunastahili Nishati Safi.










KIASHIRIA CHA JOTOARDHI SONGWE.

03.


# Kuboresha Ujuzi wa Usimamizi wa Miradi ya Jotoardhi: Mafunzo ya Watendaji wa Tanzania Nchini Japan




Katika hatua ya kuimarisha ujuzi wa wataalamu wa sekta ya jotoardhi nchini, watendaji wa Tanzania walishiriki kwenye Mafunzo ya Usimamizi wa Miradi ya Jotoardhi, yaliyofanyika nchini Japan kuanzia tarehe 6 hadi 12 Machi 2025. Hafla ya kufunga mafunzo hayo ilihitimishwa rasmi tarehe 12 Machi 2025, kwa heshima ya kuhudhuriwa na Balozi wa Tanzania nchini Japan, Mhe. Baraka Luvanda.

Mafunzo haya yaliandaliwa chini ya mwamvuli wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Wataalam wa Nje na Ubia Endelevu (AOTS) Nje na Ubia Endelevu (AOTS) kwa kushirikiana na Kampuni ya TOSHIBA, ambayo ni mshirika wa Kampuni ya Maendeleo ya Jotoardhi Tanzania (TGDC). Washiriki wa mafunzo haya walipata nafasi ya kujifunza kwa kina kuhusu teknolojia ya jotoardhi, usimamizi wa miradi, na sera za maendeleo katika sekta hii muhimu kwa nishati safi na endelevu.

Kutoka TGDC, mafunzo hayo yalihudhuriwa na Meneja Mkuu, Mha. Mathew Mwangomba, pamoja na Meneja wa Tafiti na Ubunifu, Mha. Mkufu Tindi. Kwa ujumla, watendaji wanne wa



# Kuboresha Ujuzi wa Usimamizi wa Miradi ya Jotoardhi: Mafunzo ya Watendaji wa Tanzania Nchini Japan

Tanzania wamenufaika na mafunzo haya kwa kupanua ujuzi wao na kupata mbinu bora za usimamizi wa miradi ya jotoardhi.



Huu ni mwendelezo wa juhudi za TGDC na wadau wake wa kimataifa katika kuhakikisha Tanzania inaimarisha uwezo wake wa ndani kwa ajili ya maendeleo ya nishati jadidifu. Mafunzo haya yanatarajiwa kuchochea ubunifu na kuboresha utekelezaji wa miradi ya jotoardhi nchini, kuelekea upatikanaji wa nishati safi na endelevu kwa maendeleo ya taifa.



05.

## UMEME WA JOTOARDHI KUUNGANISHWA KWENYE GRIDI YA TAIFA IFIKAPO 2030

Tanzania imelenga kuunganisha nishati ya jotoardhi kwenye gridi ya taifa ifikapo mwaka 2030 ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika unaotokana na nishati jadidifu. Lengo hili linaendana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 na azma ya kitaifa ya kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa ifikapo mwaka 2050. Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba, alibainisha haya wakati wa mkutano wa kimataifa wa Nishati Endelevu kwa Wote (SEforALL) unaofanyika Bridgetown, Barbados.



## 06. UMEME WA JOTOARDHI KUUNGANISHWA KWENYE GRIDI YA TAIFA IFIKAPO 2030

Kwa mujibu wa Mha. Mramba, mikoa 16 nchini itanufaika na maendeleo ya nishati ya jotoardhi, ikizingatiwa kuwa Tanzania ina zaidi ya maeneo 50 yenye rasilimali hii. Kampuni ya Uendelezaji ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) inaendelea na tafiti na miradi mbalimbali kuhakikisha nishati hii inachangia kikamilifu katika usambazaji wa umeme nchini. Serikali imeweka sera madhubuti za uwekezaji ili kuvutia wabia wa kimataifa kushiriki katika tafiti na maendeleo ya nishati hii.

Serikali pia imeweka mkazo kwenye mfumo wa udhibiti na sera za kuvutia uwekezaji ili kufanikisha maendeleo ya jotoardhi kama sehemu ya ajenda ya kitaifa ya nishati. Mpango huu unahusisha utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Nishati 2020 pamoja na Tamko la Dar es Salaam la "Mission 300" linalolenga kuongeza upatikanaji wa umeme kwa wote ifikapo mwaka 2030.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati wa Shirikisho la St. Kitts na Nevis, Mhe. Konris Maynard, amepongeza juhudi hizo na kusisitiza kuwa mataifa yanapaswa kukuza matumizi ya nishati safi kama jotoardhi na kuachana na nishati zinazoathiri mazingira. Tanzania, kupitia TGDC na ushirikiano wa kimataifa, inazidi kuimarisha nafasi yake kama kinara wa nishati jadidifu barani Afrika.









07.

## Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika








Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na wakuu wa nchi mbalimbali barani Afrika na viongozi wa sekta ya nishati, walishiriki Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika tarehe 28 Januari 2025 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Mkutano huu uliwaleta pamoja wadau wakuu wa nishati kwa ajili ya kujadili mbinu bora za kukuza upatikanaji wa nishati jadidifu, usalama wa nishati, na uwekezaji endelevu katika sekta ya nishati barani Afrika. Kupitia majadiliano haya ya kimkakati, viongozi walitathmini hatua zilizopigwa na kuweka mikakati mipya ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika kuendeleza nishati safi na ya uhakika kwa maendeleo ya bara la Afrika.

# 08. ZAKHEM YATEMBELEA MIRADI YA JOTOARDHI KWA FURSA ZA UWEKEZAJI

Kampuni ya Zakhem imefanya ziara ya siku tatu katika miradi ya kimkakati ya jotoardhi mkoani Mbeya na Songwe kuanzia tarehe 14 hadi 16 Januari 2025, kwa lengo la kutathmini fursa za uwekezaji katika sekta ya nishati jadidifu. Ziara hiyo iliongozwa na Mkurugenzi wa Maendeleo na Biashara wa TGDC, Mhandisi Shakiru Idrissa Kajugusi, na ilihusisha kutembelea miradi ya Ngozi, Kiejo-Mbaka, na Songwe.

Timu ya Zakhem imeonesha kuridhishwa na maendeleo yaliyofikiwa katika miradi hiyo na kuipongeza TGDC kwa juhudi zake za kuhakikisha rasilimali za jotoardhi zinachangia upatikanaji wa nishati safi na endelevu. Ziara hii imefungua milango kwa ushirikiano kati ya TGDC na Zakhem, hatua muhimu katika kuendeleza miradi ya jotoardhi nchini Tanzania.



TGDC inaendelea kushirikiana na wadau wa kimataifa na wawekezaji katika kuendeleza miundombinu ya nishati jadidifu, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kuhakikisha Tanzania inanufaika na rasilimali zake za jotoardhi kwa maendeleo endelevu. Nishati safi kwa uchumi imara!







# 09. TGDC Yashiriki Kongamano la 11 la Mafuta na Gesi Afrika Mshariki (EAPCE'25)

Kampuni ya Maendeleo ya Jotoardhi Tanzania (TGDC) ilishiriki katika Kongamano na Maonesho ya 11 ya Mafuta na Gesi Afrika Mashariki (EAPCE25) yaliyofanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Ushiriki wa TGDC katika kongamano hili ni sehemu ya mkakati wake wa kuimarisha utambulisho wake na kuvutia wawekezaji katika sekta ya nishati jadidifu, hususan jotoardhi.

Katika banda la TGDC, kampuni hiyo ilipata heshima ya kutembelewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Alipata fursa ya kujifunza na kupata taarifa za kina kuhusu hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya jotoardhi nchini Tanzania.

Kama mdau muhimu katika sekta ya nishati jadidifu Tanzania, TGDC imejikita katika kuchochea maendeleo ya nishati safi kupitia rasilimali za jotoardhi ili kuchangia maendeleo endelevu na usalama wa nishati katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kongamano hili lilitoa fursa adhimu kwa TGDC kushiriki mijadala ya kina na viongozi wa sekta, watunga sera, na wawekezaji wanaoshiriki maono ya kukuza nishati mbadala kwa maendeleo ya kikanda.

Kupitia maonesho haya, TGDC ilijadili mambo muhimu kuhusu maendeleo ya jotoardhi, ilipanua mtandao wa ushirikiano, na kuchunguza fursa mpya za ubia ambazo zitaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya jotoardhi nchini. Ushiriki wa TGDC katika kongamano hili ni hatua muhimu katika kuhakikisha Tanzania inatumia kikamilifu rasilimali za jotoardhi kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii.





JOTOARDHI SPA
SONGWE.

## 10. TGDC Yawahamasisha Nsongwi Juu, Nsenga na Mbeye1, Utunzaji, Upokeaji na Ulindaji Mradi wa Jotoardhi Ngozi

Katika kuimarisha ushirikiano, ulinzi na umilikishwaji wa miradi kwa wananchi na kuwafanya waitunze na kuipa kipaumbele cha utunzaji katika sehemu iliyopita mradi wa jotoardhi Ngozi, Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imefanya ziara ya uhamasishaji na uelimishaji katika vijiji vya Nsongwi Juu, Nsenga na Mbeye1, ikiwa ni sehemu ya juhudi zake za kuimarisha uhusiano na jamii zinazouzunguka mradi wa Jotoardhi Ngozi. Ziara hiyo imefanyika mfululizo kuanzia Machi 17 hadi 20, 2025 kwa nyakati tofauti ambapo wakazi wa maeneo hayo walinufaika na elimu iliyotolewa na kuonesha utayari wao katika kuipokea na kuilinda miundombinu inayozunguka miradi ya jotoardhi.

Wakiwa katika vijiji hivyo vitatu kwa nyakati tofauti, wataalam kutoka TGDC ambao ni Bi. Khadija Ahmed, Mhandisi Luhinda Luyagwa, Mhandisi Esther Range, Bw. Juma Mpamba, Bw. Boaz Mazigo, Bw. Joshua Nelei, Bw. Omary Seleman na Bw. Leonce Komba walitoa elimu ya ufahamu na umuhimu wa utunzaji wa mradi pindi shughuli za uchimbaji zitakapoanza kwa ajili ya uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi ikiwa ni safari kuelekeza uzalishaji umeme utokanao na rasilimali ya jotoardhi.

Katika mawasilisho yao, watalaam walisisitiza juu ya umuhimu wa wananchi kuiona miradi na miundombinu yote iliyowekwa na itakayowekwa kama miradi yao wakiilinda na kwakuwa inatekelezwa na Serikali itawanufaisha wananchi wote wakiwemo wa maeneo yanayozunguka mradi, hivyo wanapaswa kuilinda. Pamoja na mengine, waliahidiwa kuwa sehemu ya watekeleza mradi kupitia ajira zitolewazo kwa kuzingatia wazawa ikiwemo vibarua, walinzi n.k pindi utekelezaji utakapoanza.

Mwisho, kila mmoja aliombwa kuwa mlinzi wa mazingira kwa kuwa miongoni kwa kampeni ya TGDC ni utunzaji wa mazingira na hata umeme wa jotoardhi utakapozalishwa hautachafua mazingira bali ni rafiki wa mazingira. Vilevile, waliombwa kuwa na mawasiliano ili inapotokea changamoto yoyote basi iwe rahisi kutatuliwa.

Kwa upande wa wananchi wa Nsongwi Juu, waliishukuru TGDC kwa elimu iliyotolewa na walihitaji ufafanuzi wa masuala mbalimbali ikiwemo ni kwa jinsi gani wazee wenyeji walivyoyatunza mazingira watanufaika na mradi, utoaji vipaumbele vya ajira kwa wazawa na uboreshwaji wa miundombinu ya barabara, mambo ambayo yalitolewa ufafanuzi kwa kuhakikishiwa ajira pamoja na uboreshaji wa barabara.

# 11

# TGDC Yawahamasisha Nsongwi Juu, Nsenga na Mbeye1, Utunzaji, Upokeaji na Ulindaji Mradi wa Jotoardhi Ngozi

Wananchi wa Kijiji cha Nsenga nao waliuliza juu ya namna ya kunufaika na mradi ikiwemo ajira kwa vijana, pamoja na miundombinu ya barabara, jambo ambalo lilitolewa ufafanuzi na kuhakikishiwa ajira za muda wakati wa utafiti na za moja kwa moja wakati wa uzalishaji, uboreshwaji miundombinu pamoja na mashirikiano baina ya TGDC na wananchi

Katika Kijiji cha Mbeye 1 waliishukuru TGDC kwa namna ambavyo imekuwa mstari wa mbele kuunga mkono shughuli za jamii ya wana Mbeye1 ikiwemo kupeleka maji katika Shule ya Msingi Mbeye1, jambo lililowapunguzia ajali wanafunzi waliokuwa wakivuka barabara kwa ajili ya kufata maji. Pia ugawaji mabegi kwa wanafunzi wa shule hiyo pamoja na vifaa kama daftari.

Katika hatua nyingine, wana Mbeye1 walilaani uharibifu wa miundombinu ambao hufanywa na watu wasio waaminifu na wao kuahidi kuendelea kuwa mabalozi wazuri wa kuilinda miundombinu ya TGDC, huku wakiiomba TGDC kuendelea kuishika mkono kwenye ujenzi wa zahanati na madarasa ya shule pamoja na miundombinu ya barabara; mambo ambayo wataalam wa TGDC waliahidi kuyashughulikia kwa ukaribu katika kuyajadili katika ngazi ya maamuzi.


TGDC iko mbioni kuhakiki rasilimali ya jotoardhi katika miradi ya kipaumbele mitano ya Ngozi na Kiejo-Mbaka (Mbeya), Songwe (Songwe), Luhoi (Pwani) na Natron (Arusha) yenye lengo la kuzalisha Megawati 200 za umeme ifikapo 2030. Kwa sasa itaanza na mradi wa jotoradhi Ngozi (70Mw) ambapo baada ya uhakiki, hatua ya uzalishaji itafuata.

Na kwa kufanya hivi, TGDC itakuwa imechangia umeme kwenye gridi ya Taifa unaotokana na nishati safi isiyoharibu mazingira.

TGDC, Tunastahili Nishati Safi







ZIWA NGOZI, MBEYA

# TGDC Yajengewa Uwezo Katika Sheria Mpya ya Manunuzi ya 2023 na Kanuni za 2024



Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti,Bodi ya Zabuni, na baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) walikutana mjini Iringa kuhudhuria mafunzo ya sheria mpya ya manunuzi ya mwaka 2023 pamoja na kanuni zake za mwaka 2024.

Lengo likiwa kuwajengea uwezo katika kusimamia na kutekeleza mpango wa kampuni kwa kuzingatia sheria za nchi. Mafunzo haya yalianza tarehe 24 machi na yatamalizika tarehe 27 Machi, 2025 katika Hoteli ya Mount Royal, Iringa.





13

# Wafanyakazi 12 wa TGDC Wala Kiapo, Wanolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma-Mbeya



Jumla ya watumishi kumi na mbili (12) wa Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) walikula kiapo cha maadili ya utumishi wa umma na kupatiwa mafunzo kama zilivyo taratibu kwa mtumishi yeyote wa umma pindi anapoajiriwa.

Mafunzo hayo ya siku nne yalitolewa na Chuo cha Utumishi wa umma kuanzia tarehe 24 hadi 27 Februari, 2025 katika ukumbi wa Hoteli ya Beaco iliyopo Mbeya mjini ambapo washiriki walipata fursa kujifunza mada mbalimbali wakati wa mafunzo hayo ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu na uendeshaji wa ofisi, mapitio ya Sheria ya utumishi wa umma Na.8 ya mwaka 2022, kanuni za kudumu za utumishi wa umma za mwaka 2009, Muundo wa Serikali na uendeshaji wa shughuli zote, jinsi ya kujiandaa kustaafu n.k.

Akiongea na washiriki hao wakati akitoa mada, bw. John Stephen, Mkufunzi kutoka chuo cha Utumishi wa Umma – Mbeya alisema, "ni muhimu kuzingatia sheria zinazosimamia utendaji kazi katika utumishi wa umma na endapo mkikiuka, zipo adhabu kulingana na kosa husika. Hivyo zinagtieni haya tuliyowaelekeza".

Kwa upande wa mwakilishi na mratibu wa mafunzo kutoka Idara ya Rasilimali watu na Utawala TGDC Bi. Swalha Soka alisisitiza umuhimu wa mafunzo hayo yaliyowezeshwa na ofisi ya Meneja Mkuu wa TGDC ambaye anayatambua kwa kuwaeleza washiriki kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, utunzaji siri, kanuni, sheria, taratibu na miongozo yote ili waweze kuendana na matakwa ya ajira zao.

Mwisho, washiriki wote walikula kiapo kulinda maadili na kanuni za utumishi wa umma kama inavyostahili.

Huu ni utaratibu wa kawaida wa Serikali kuwawezesha watumishi waajiriwa wapya ambapo TGDC imeendelea kutekeleza wajibu huu ili kuendana na matakwa ya Serikali katika kuhakikisha Serikali inafanya kazi kama zilivyopangwa.



Jotoardhi Jarida: Toleo la Robo ya Tatu (2024/2025)

Limethimitishwa na:

Mha. Mathew Mwangomba

## Imeandaliwa na:

IDARA YA MAWASILIANO - TGDC

Khadija Ahmed - Mkuu wa Idara

Boaz Mazigo - Afisa Mawasiliano Mwandamizi

Leonce Komba - Afisa Mawasiliano

TgdcTanzania

www.tgdc.go.tz